PRESS RELEASE

PR25/112

# Ujumbe wa Wafanyakazi Kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) wakamirisha Majadiliano ya Mwaka 2025 Chini ya Kanuni ya Nne ya Mkataba Ulioanzisha Shirika hilo (Article IV Consultation) na pia Kufikia Makubaliano ya Ngazi ya Wafanyakazi na Serikali ya Tanzania Kuhusu Tathmini ya Tano ya Utekelezaji wa Mpango wa Ukopeshaji wa ECF (Extended Credit Facility) na Tathmini ya Pili ya Utekelezaji wa Mpango wa Ukopeshaji wa RSF (Resilience and Sustainability Facility)

**FOR IMMEDIATE RELEASE**

End-of-Mission press releases include statements of IMF staff teams that convey preliminary findings after a visit to a country. The views expressed in this statement are those of the IMF staff and do not necessarily represent the views of the IMF's Executive Board. Based on the preliminary findings of this mission, staff will prepare a report that, subject to management approval, will be presented to the IMF's Executive Board for discussion and decision.

- Shirika la Fedha la Kimataifa limefikia makubaliano ya ngazi ya wafanyakazi na serikali ya Tanzania kuhusu tathmini ya tano ya mpango wa ukopeshaji wa ECF (Extended Credit Facility) na tathmini ya pili ya mpango wa ukopeshaji wa RSF (Resilience and Sustainability Facility). Tanzania itapata ufadhili wa dola za Marekani milioni 441 mara baada ya tathmini hizi kuidhinishwa na Bodi Tendaji ya IMF.
- Matarajio ya uchumi wa Tanzania ni mazuri kwakuwa utaendelea kukua kwa kasi, huku mfumuko wa bei ukiendelea kuwa chini, nakisi ya mauzo na manunuzi ya bidhaa na huduma nje ya nchi ikipungua, na upatikanaji wa fedha za kigeni ukiongezeka. Hatua za kuwianisha vizuri mapato na matumizi ya serikali katika mwaka wa fedha wa 2025/26, zitasaidia kuhifadhi uhimilivu wa deni la serikali, huku zikilinda matumizi yenye kipaumbele katika huduma za kijamii.
- Kuendelea kutekeleza sera za kukabiliana na athari na changamoto za mabadiliko ya tabianchi, zinazoungwa mkono na mpango wa RSF, kutasaidia kujenga ustahimilivu katika kushughulikia madhara ya mabadiliko ya tabianchi.

**Washington, DC - Aprili 17, 2025:** Ujumbe wafanyakazi kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) wakiongozwa na Bw. Nicolas Blancher, walitembelea Tanzania wakati wa Aprili 2-17, 2025, na kufanya majadiliano ya mwaka 2025 chini ya kanuni ya nne ya mkataba ulioanzisha shirika hilo (Article IV Consultation), na pia kufanya tathmini ya tano ya mpango wa ukopeshaji wa ECF (Extended Credit Facility) na tathmini ya pili ya mpango wa ukopeshaji wa RSF (Resilience and Sustainability Facility). Endapo tathmini hizi zitaidhinishwa na Bodi Tendaji ya IMF, zitapelekea kupatikana kwa SDR 326.47 milioni (kama dola za Marekani milioni 440.8), na kufanya jumla ya ufadhili wa kifedha wa IMF chini ya mpango wa ECF kufikia SDR milioni 682.21 (kama Dola za Marekani milioni 907.4), na SDR 255.72 milioni (kama dola milioni 343) chini ya mpango wa RSF.

700 19th Street NW
Washington, DC 20431
USA

Mwishoni mwa ziara yake, Bw. Blancher, ametoa taarifa ifuatayo:

"Ninafurahi kutangaza kwamba ujumbe wa wafanyakazi kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa wamefikia makubaliano ya ngazi ya wafanyakazi na serikali ya Tanzania kuhusu tathmini ya tano ya utekelezaji wa sera zinaoungwa mkono na mpango wa ECF, na tathmini ya pili ya utekelezaji wa sera zinaoungwa mkono na mpango RSF. Bodi Tendaji ya IMF inategemea kujadili tathmini hizi katika wiki zijazo.

"Shughuli za kiuchumi nchini Tanzania zimeimarika, na ukuaji halisi wa Pato la Taifa umefikia asilimia 5.5 mwaka 2024 na unatarajiwa kuongezeka hadi asilimia 6 mwaka 2025. Mfumuko wa bei, kwa asilimia 3.3 mwezi Machi (mwaka hadi mwaka) bado upo chini na umeendelea kuwa chini ya lengo la Benki Kuu ya Tanzania la asilimia 5. Wakati matarajio ya kiuchumi ni mazuri, athari za kiuchumi zinaongezeka. Mazingira ya kiuchumi nje ya nchi siyo mazuri kutokana na kushuka kwa uchumi na biashara duniani, mgawanyiko wa kiuchumi kijiografia, kuongezeka zaidi kwa mzozo katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, na kupungua kwa misaada ya maendeleo. Kwa upande wa ndani ya nchi, uchaguzi mkuu ujao unaweza kuongeza shinikizo la kufanya matumizi zaidi au, kwa upana zaidi, kupunguza kasi ya mageuzi.

"Kubana matumizi ya serikali kunatarajiwa kusitishwa katika mwaka wa fedha 2024/25 baada ya kupitishwa bajeti ya ziada mwezi Februari 2025 yenye lengo la kuongeza matumizi ya umma kwa takriban asilimia 0.4 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na bajeti ya awali, ili kuongeza matumizi kwenye elimu na afya, kulipa malimbikizo ya madeni, na maeneo mengine ya kipaumbele. Itakuwa muhimu sana kuanza tena kupunguza matumizi mwaka wa fedha 2025/26 ili kuhifadhi uhimilivu wa deni la serikali na kujenga upya nafasi ya kuongeza matumizi hapo baadaye, haswa kwa kuzingatia mahitaji makubwa ya matumizi sekta za kijamii. Serikali imejitolea kupunguza nakisi ya msingi ya ndani ya bajeti kwa asilimia 0.4 ya Pato la Taifa hadi asilimia 0.8 katika mwaka wa fedha 2025/26 kupitia hatua za kuongeza mapato ya ndani zitakazozalisha asilimia 0.9 ya Pato la Taifa, huku matumizi ya kipaumbele ya kijamii yakiendelea kulindwa na kubakia kwenye asilimia 7.1 ya Pato la Taifa.

"Pamoja na mfumuko wa bei kusalia chini ya lengo la asilimia 5 la Benki Kuu ya Tanzania, kubakiza Riba ya Benki Kuu kwenye asilimia 6, kiwango ambacho ujumbe wa wafanyakazi toka IMF unaona hakiegemei upande wowote au ni kichocheo kidogo, kutasaidia kuhifadhi uthabiti wa bei katika kipindi kijacho. Pia itakuwa muhimu kuendelea kuruhusu viwango vya kubadilisha fedha za kigeni ili vitokane na nguvu za soko na Benki Kuu ya Tanzania iingie kwenye soko la fedha za kigeni kulingana na sera yake ya uingiaji kwenye soko hilo. Kuongezeka kwa uvumilivu wa viwango vya kubadilisha fedha za kigeni vinavyotokana na nguvu za soko na mageuzi ya kuboresha utendaji wa soko la fedha za kigeni imesidia kurudisha fedha za kigeni katika soko rasmi na hivyo kupunguza biashara ya fedha za kigeni katika soko lisilo rasmi.

"Nakisi ya mauzo na manunuzi ya bidhaa na huduma nje ya nchi inakadiriwa kuwa imepungua hadi asilimia 2.6 ya Pato la Taifa katika mwaka 2024, kutoka asilimia 3.8 ya Pato la Taifa katika mwaka 2023. Hii ilitokana na mauzo mazuri nje ya nchi ya madini na mazao ya kilimo, pamoja na idadi kubwa ya watalii waliofika, dhidi ya ongezeko la wastani la uagizaji wa bidhaa za uwekezaji na kupungua kwa uagizaji wa mafuta nje ya nchi. Katika mwaka 2025, bei nzuri ya dhahabu inatarajia kuongeza mauzo ya nje na hivyo kusaidia kupunguza nakisi ya mauzo na manunuzi ya bidhaa na huduma nje ya nchi. Akiba ya fedha za kigeni ilifikia kiwango cha kutosha cha Dola za Marekani bilioni 5.7 (kama miezi 3.8 ya uagizaji bidhaa kutoka nje) mwezi Machi 2025."

"Katika muktadha wa majadiliano ya mwaka 2025 chini ya kanuni ya nne ya mkataba ulioanzisha shirika la IMF (Article IV Consultation), ujumbe wa wafanyakazi pia ulipata fursa ya kujadiliana na wadau mbalimbali toka serikalini na washirika wengine kuhusu matarajio ya muda mrefu ya uchumi wa Tanzania. Ili kufikia malengo makubwa yaliyoainishwa katika Dira ya Tanzania ya 2050, ni muhimu kuhakikisha kuwa rasilimali za kutosha zinatolewa kwa ajili ya elimu na afya ya vijana na idadi kubwa ya watu inayokua kwa kasi, na kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kukuza na kuboresha sekta binafsi ili kuongeza kasi ya ukuaji wa ajira. Hasa upatikanaji wa mikopo ya kifedha, kuhuisha kanuni za biashara, na kuimarisha taasisi za mahakama na kupambana na rushwa, hivi ni vipaumbele muhimu vya mageuzi ya kimuundo.

"Kuendeleza utekelezaji wa mageuzi katika sekta za mazingira na hali ya hewa yanayoungwa mkono na RSF, kutaongeza uwezo wa kuhimili athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi. Serikali tayari imeanza kuimarisha mfumo wa kitaasisi wa sera za tabianchi na usimamizi wa uwekezaji wa umma kwa kuzingatia athari za mabadiliko ya tabianchi.Kuharakisha utekelezaji wa mageuzi ya RSF kwa msaada wa kiufundi na kifedha kutoka IMF, Benki ya Dunia, na washirika wengine wa maendeleo, kutasaidia kujenga uwezo wa kustahimili mabadiliko tabianchi na kuchochea ufadhili kwa Tanzania kwenye masuala hayo.

"Ujumbe wa wafanyakazi toka IMF ulikutana na Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba, viongozi wengine waandamizi wa serikali, washirika wa maendeleo, wawakilishi wa sekta binafsi na mashirika ya kiraia. Wajumbe wanapenda kuzishukuru mamlaka za Tanzania na wadau wengine kwa ukarimu wao, na majadiliano ya dhati na yenye tija."